FOOTSTEPS

No.32 SEPTEMBER 1997

FOOD SECURITY

Wanawake wa vijijini na swala la lishe

na Drs Neela na Amitava Mukherjee

Miongoni mwa watu takriban milioni 350 wanoishi katika hali ya umaskini nchini India, swala la chakula au lishe ni la kufa kupona. Shughuli za kilimo ni uti wa zaidi ya 70% ya idadi ya watu nchini India, idadi kubwa ya watu hao wana mashamba chini ya hekta 2.

Tunaamini na kutambua kwamba jamii au kundi la watu lina lishe la kutosha iwapo:

- aina ya chakula kinachokubaliwa katika mila na desturi kinakuzwa kwa wingi
- watu wanao uwezo wa kununua vyakula
- watu wanao uwezo wa kuchagua na kununua chakula wanachopenda
- Chakula kilichoko kina virutubishi vifaavyo

Kuna aina tatu ya vyakula vilivyoko kwa wakulima wa kiwango kidogo:

- vyakula vinavyoweza kuchunwa pasipo mavuno
- vyakula vya kiasili, vilivyohitaji gharama kuu katika kukuza - kilimo kisicho ghali
- vyakula kutoka kwa mashamba yanayo zingatia mfumo wa kisasa (kwa kutumia mbolea, madawa ya kukabili wadudu na mashine ya kisasa) - mfumo wa gharama.

Miongo miwili iliyopita, kiwango cha nafaka (kama ngano, mchele na mahindi) kutoka kwa mifumo ya kilimo kilichoimarishwa kimeongezeka mara tatu au nne nchini India. Hata hivyo kiwango cha mazao ya jamii ya kunde na maharagwe kimepungua, chanzo kikuu cha protini kwa jamii fukara.

KATIKA TOLEO HILI

- Akiba ya nafaka kwa jamii
- Barua
- Hifadhi la nafaka
- Kuhifadhi na kutunza vyakula
- Aina ya ghala lililoimarishwa
- Uchachuzi
- Kukabili ukame
- Kutayarisha jemu
- Somo la Bibilia: Kiwango cha kutosheleza ni sawa na karamu
- Marejeleo
- Kuendeleza hifadhi

Hali hii imechangia kubadili kwa mfumo wa lishe. Aina ya nafaka ya jadi na kiasili imeangamia na mahali pake kuchukuliwa na mchele na ngano. Hata aina ya mchele na ngano ya kiasili umeangamia. Maana ya kipengele cha kwanza - aina ya chakula kinachokubaliwa baina ya itikadi na desturi za jamii - kinapungua kwa haraka. Mfumo wa kilimo cha kisasa unaelekeza wakulima wengi kujilimbikizia madeni huku wakijaribu kununua vifaa vinavyohitajika. Kipengele cha pili pia kinatishwa, kwani uwezo wa wakulima kununua vyakula umepungua.

Photo: Santosh Verma

FOOTSTEPS

ISSN 0962-2861

Footsteps ni jarida linalotolewa kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya wahudumu wa afya na maendeleo ya jamii. Shirika la TearFund, ndilo huchapisha makala haya, na latumaini kwamba maelezo haya yanasisimu. Hii ni mojawapo ya mbinu ya mawasiliano kwa Wakristo wa mataifa yote katika kutafuta usawa wa jamii.

Footsteps hutolewa bure pasipo malipo ili kuendelezais afya bora na maelezo ya maendeleo ya jamii. Jarida hili hupatikana kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kiispania. Toleo au ufadhili hukaribishwa. Wasomaji aidha wanaombwa kuchangia kwa maoni, barua na picha

Mhariri: Isabel Carter
83 Market Place, South Cave, Brough, East Yorkshire, HU15 2AS, UK.
Tel/Fax: (0)1430 422065
E-mail: imc@tearfund.dircon.co.uk

Mhariri wa Lugha: Sheila Melot

Kamati ya Kuhariri: Jerry Adams, Dr Ann Ashworth, Simon Batchelor, Mike Carter, Jennie Collins, Bill Crooks, Paul Dean, Richard Franceys, Dr Ted Lankester, Sandra Michie, Nigel Poole, Louise Pott, José Smith, Mike Webb

Mchoraji: Rod Mill

Ubunifu: Wingfinger Graphics, Leeds

Tafsiri: L Bustamante, R Cawston, Dr J Cruz, S Dale-Pimentil, S Davies, T Dew, N Edwards, J Hermon, J Martinez da Cruz, R Head, M Leake, M Machado, O Martin, N Mauriange, J Perry

Anwani: Tuma ombi kwa kutoa maelezo ya mukhtasari kuhusu kazi yako na lugha unayohitaji kupokea makala, kwa:
Footsteps Mailing List, Tear Fund, 100 Church Road, Teddington, Middlesex, TW11 8QE, UK. (Tel: (0)181 977 9144.)

Kubadilisha anwani: Tafadhali nukuu nambari iliyo kwenye bahasha kila mara unapobadili anwani.

Maelezo na michoro kutoka kwa *Footsteps* yanaweza kutumiwa na wahudumu katika kufundisha, sharti haki ziheshimiwe na kunukuu *Footsteps*, TearFund. Ruhusa au idhini yapaswa kuombwa kabla ya kunakili *Footsteps*.

Maoni na maelezo yaliyo kwenye barua za wasomaji sio yale ya mhariri au shirika la Tear Fund. Maelezo yote ya kiufundi au aina nyingine huchunguzwa kwa makini, hata hivyo hakuna dhamana kutoka kwa shirika hili endapo tatizo litatokea.

Chapisho la Tear Fund. Kampuni ya dhamna. Regd in England No 994339.

Regd Charity No 265464.

TEAR FUND
CHRISTIAN CONCERN IN A WORLD OF NEED

Usalama wa lishe ni hali ya watu kuwa huru kununua na kuchagua chakula bora.

Wanawake ndio huadhiriwa zaidi kadri chakula kinapo pungua. Wanaweza kulazimika kufanya kazi kwa saa nyingi nje ya mazingara yao huku wakitafuta fedha za kukimu uhaba wa lishe. Wanawake wanajukumu la kugawa chakula kwa jamii na hivyo basi kujinyima ili kuhakikisha watoto wanapata lishe la kutosha.

Vyakula vya kutafutwa hutumiwa nyumbani au hata kuuzwa. Vyakula kama hivi vina virutubishi vya vitamini na madini muhimu. Wakati wa kiangazi, ukame au janga lingine, vyakula hutafutwa, hivyo basi kujulikana kama 'vyakula vya njaa'.

Takwimu chache huonyesha kiasi cha chakula kinachotafutwa. Utafiti uliofanywa na N S Jodha (1986) katika sehemu kame nchini India ulibaini kwamba theluthi moja ya hitaji la vyakula vilipatikana kwa mfumo huu.

Utafiti wa kubadili usalama wa lishe

Utafiti mwingine umebainisha kwamba ni wanawake ndio wanaodhibiti kuwepo kwa chakula nyumbani na hutafuta mboga na vyakula hata msituni. Ongezeko la kiasi cha nafaka nchini India sio suluhisho la tatizo la lishe kwa watu maskini.



Photo: Richard Hanson, Tear Fund

Hali hii yaweza kubainishwa wazi kutokana na utafiti uliofanywa katika kijiji cha Krishna Rakshit Chak, Wilaya ya Midnapore, magharibi mwa Bengal. Wakaazi wa eneo hilo ni tabaka la Lodha lenye umaskini na ukosefu wa shamba. Utafiti ulihusisha akina mama wa eneo la Krishna Rakshit Chak ili kuelewa:

- Maarifa yao kuhusu vyakula vya msitu
- Jukumu lao katika kutafuta vyakula msituni
- Kuwepo kwa vyakula katika msimu fulani
- Jinsi idadi ya vyakula vya msitu imepungua kadri siku zinavyo songa.

Wanawake walihimizwa kuandaa kalenda za msimu na aina ya vyakula vilivyoko. Kwa kutumia mawe madogo walionyesha idadi ya chakula kwa mwaka mzima. Kisha kutumia majani, vijiti na matawi ya kila aina kuonyesha matumizi ya aina mbalimbali ya vyakula vya kutafutwa. Katika kadirio hilo, kiasi au idadi iliyotumiwa ilikuwa ya kubahatisha.

Watafiti kisha wakarudi baada ya miaka miwili mnamo 1995, wakati ambao wanawake waliombwa kutayarisha kalenda ili kuonyesha tofauti zilizotokea.

Matokeo

Wanawake waliweza kutambua aina ya vyakula vya msitu kulingana na msimu. Ni jukumu lao kutafuta na hatimaye kutayarisha vyakula kama hivyo.

Kila aina ya kalenda ilionyesha kipindi kirefu cha njaa. Licha ya tarakimu za serikali zinazoonyesha kiwango kikubwa cha mavuno kutoka kwa mifumo ya kisasa. Mnamo mwaka wa 1995, msimu wa njaa ulikuwa mrefu na wenye maafa mengi zaidi. Iligunduliwa kwamba kinyume na tarakimu rasmi, watu maskini walikumbwa na uhaba wa chakula mwaka wa 1995 kuliko mwaka wa 1993.

Wakaazi wa vijiji walipendelea mchele kama chakula kikuu. Matumizi ya mchele yalitegemea bei na uwezo wao wa kupata kazi ili waweze kununua. Baada ya mavuno (Argrhayan na Poush - katikati ya Novemba hadi Januari), bei ilipungua na idadi ya mazao kuongezeka. huo ndio wakati mchele ulitumiwa kwa wingi. Bei ya mchele iliamua aina ya chakula kingine kinachoweza kununuliwa.

Wakaazi waliweza kupata ujira wakati wa mavuno na baadaye wakati wa kuwembua na kutayarisha mchele. Wakati huo bei ilipungua huku watu wakiwa na pato kutokana na ujira, wakaazi walikuwa na uwezo wa kununua mchele utakao tumiwa kwa miezi kadhaa.

Kadri shughuli za kilimo zinapopungua, wakaazi waliuza samaki na kuni na kutumia nafaka iliyo hifadhiwa. Baadaye mwakani maisha huanza kuwa magumu, bei ya chakula kikuu huongezeka, ikifuatia na miezi mingi ya njaa huku watu wakitegemea vyakula vya msitu. Kati ya mwaka wa 1993 n 1995, kipindi cha msimu wa njaa kiliongezeka kutoka miezi 5 hadi miezi 8. Mnamo mwaka wa 1995, chakula kutoka kwa msitu kilipungua.

Wakaazi waliulizwa mbona vyakula vya msitu (kama vile konokono, malenge, mdewere, majani, ndizi na mimea ya maji) vilipungua mwaka wa 1995, maelezo yao yalivutia.

Kwanza walisema mnamo mwaka wa 1993, waliweza kuingia kwenye mashamba ya watu matajiri. Kisha wakulima hao matajiri wakawa na tamaa ya kuuza chochote kilichokuwa shambani hata vyakula vya njaa.

Pili walieleza kwamba, mashamba ya uma yanapungua. Mashamba kama hayo yanageuzwa na kuwa hifadhi la misitu. Hivyo basi akina mama na watoto wanatembea mwendo mrefu kutafuta vyakula vya msitu.

Hitimisho

Licha ya ripoti na maelezo rasmi kuhusu ‘mavuno bora’ na kuimarika kwa hali ya uchumi, njaa imeongezeka katika kijiji hiki.

Kupoteza kwa uwezo wa kuingia msituni au katika baadhi ya mashamba kutafuta vyakula kumechangia muda mrefu wa njaa. Serikali ingalisaidia kwa kuchimba vidimbwi vya kukuza samaki na kunyunyiza maji. Hata hivyo, msaada huo uliendea wamiliki wa mashamba. Msaada kwa watu maskini wasio na mashamba ndilo suluhisho kwa jamii za kijiji hiki.

Dr Neela Mukherjee Ni Profesa wa maswala ya Uchumi katika Talmia ya Kitaifa ya Usimamizi, Mussoorie, UP 248 179, India. Mumewe Dr Amitava Mukherjee, ni Mkurugenzi mkuu wa Action Aid India, 3 Rest House Road, PO 5406, Bangalore 560 001, India.

Mhariri

Waweza kujaribu utafiti huu katika eneo lako ili kufahamu na kuelewa matatizo ya usalama wa lishe?

KUTOKA KWA MHARIRI

MATAYARISHO YA TOLEO HILI yalianza kwa dhamira ‘kuhifadhi mavuno’. Lakini tukaona ni muhimu kupanua dhana hiyo ili kuangazia usalama wa lishe, mada iliyozua maswala mengi. Maana kamili ya usalama wa lishe ni kama alivyoeleza von Braun (1992): ‘*Uwezo wa kila mtu kupata chakula kwa wakati wowote kwa viwango vinavyohitajika kila mara ili kuishi maisha bora yenye afya*’. Kwa kutambulikana watu milioni 800 kote duniani walio na njaa, watoto milioni 190 walio na utapiamlo na uzani duni, watoto milioni 230 wasio na ukuaji wa kawaida, mbali na watu bilioni 2 walio na matatizo ya virutubishi - ni wazi na bayana kwamba idadi kubwa ya waatu ulimwenguni imeadhiriwa pasipo kufurahia usalama wa lishe.

Robo tatu ya watu walio na matatizo ya **ukosefu** wa lishe wanaishi katika vijiji. Drs Mukherjee wamepambanua kinaganaga kuhusu tabaka fulani nchini India, sio tofauti na vijiji vingine maskini katika sehemu nyingine duniani. Kutoka Afrika kuna maelezo kuhusu akiba ya nafaka na maelezo ya kuendeleza warsha ili kuangazia usalama wa lishe.

Kutoka Amerika Kusini, Miges Baumann ameangazia tisho la kuangamia kwa vyakula vya kiasili.

Tangu jadi kulingana na desturi, wanaume hutunza ghala, huku wanawake wakishughulikia chakula cha siku kwa siku. Wanawake huangaika huku wakitafuta chakula cha kila siku. Ni wazi kwamba wanawake watatumia pato lao kwa chakula mara moja kuliko wanaume. Tunaangazia hifadhi la nafaka na hifadhi la vyakula kwa jumla, ili kutoa maelezo rahisi ya kuzingatia.

Usalama wa lishe ni jambo linalojadiliwa katika viwango vya serikali au hata katika kongamano la kimataifa. Hata hivyo tunaamini kwamba swala la usalama wa lishe litafaulu iwapo chakula kitapatikana **katika vijiji, kutayarishwa, kuhifadhiwa na kugawa.** Kuna aina mbali mbali ya mada ambazo zingalijadiliwa, hata hivyo ni tumaini letu kwamba maelezo haya ni ya manufaa ili uweze kutafakari zaidi. Tunahimiza ufuate maelezo na mbinu za Pukuta Mwanza, na kuanzisha kundi la majadiliano au warsha ya usalama wa lishe katika kijiji au mji wako.

Isabel Carter